BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KIDATO CHA PILI (FTNA) 2018

# 015 ELIMU YA DINI YA KIISLAMU

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KIDATO CHA PILI (FTNA) 2018

# 015 ELIMU YA DINI YA KIISLAMU

Kimechapishwa na
Baraza la Mitihani la Tanzania
S.L.P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania

**© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2019**

Haki zote zimehifadhiwa

## YALIYOMO

DIBAJI ..... iv

1.0 UTANGULIZI ..... 1

2.0 TATHMINI YA KILA SWALI KWA MADA ..... 2

2.1 SEHEMU A: SUNNAH NA HADITHI NA TAWHIID ..... 2

2.1.1 Swali la 1: Sunnah na Hadithi-Uchaguzi wa Majibu Sahihi ..... 2

2.1.2 Swali la 2: Tawhiid - Kuoanisha Maneno na Sentensi ..... 7

2.2 SEHEMU B: TAWHID, TAREKH NA QUR'AN ..... 11

2.2.1 Swali la 3: Tawhiid - Kujibu Kweli au si Kweli ..... 12

2.2.2 Swali la 4: Tarekh - Kujaza Nafasi Zilizowazi ..... 15

2.2.3 Swali la 5: Qur'an - Kupanga Nukuu Katika Mpangilio sahihi ..... 19

2.3 SEHEMU C: FIQH ..... 22

2.3.1 Swali la 6: Fiqh - Kujibu kwa Ufupi ..... 23

2.3.2 Swali la 7: Fiqh - Insha ..... 30

3.0 UCHAMBUZI WA KUFAULU KWA KILA MADA ..... 34

4.0 HITIMISHO ..... 34

5.0 MAPENDEKEZO ..... 35

Kiambatisho ..... 36

# DIBAJI

Taarifa ya Uchambuzi wa Majibu ya Wanafunzi katika Maswali ya Upimaji wa Kidato cha Pili (FTNA) 2018 kwa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu imeandaliwa kwa lengo la kutoa mrejesho kwa wanafunzi, walimu, watunga sera, wadhibiti ubora wa elimu, watunga mitaala na wadau wengine wa elimu kuhusu namna wanafunzi walivyojibu maswali ya upimaji huo. Majibu ya wanafunzi katika upimaji ni kiashiria kimojawapo kinachoonesha mambo ambayo wanafunzi waliweza kujifunza kwa usahihi na yale ambayo hawakuweza kujifunza katika kipindi cha miaka miwili ya kwanza ya Elimu ya Sekondari.

Uchambuzi kwa kila swali umefanyika ambapo dosari mbalimbali zilizojitokeza katika majibu ya maswali zimeainishwa kwa kuonesha wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi. Uchambuzi huu umeonesha jinsi wanafunzi walivyopata alama za juu, wastani na chini kwa kila swali na sampuli za majibu ya wanafunzi waliofanya vizuri au vibaya zimeoneshwa. Aidha, sababu mbalimbali ambazo zilichangia wanafunzi kuweza au kushindwa kujibu maswali kwa usahihi zimebainishwa. Sababu zilizowafanya baadhi ya wanafunzi kuweza kujibu maswali kwa usahihi ni kama vile uelewa wa matakwa ya maswali na kuwa na maarifa ya kutosha ya mada mbalimbali za somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu. Aidha, uchambuzi umeonesha kuwa baadhi ya wanafunzi walishindwa kujibu maswali kwa usahihi kutokana na kutotambua matakwa ya maswali na kuwa na maarifa finyu katika mada mbalimbali na hasa kuhifadhi na kutafsiri Qur'an na Fiqh (Hijja). Uchambuzi umebaini kuwepo kwa udhaifu katika kujibu maswali ya kujieleza na mpangilio wa kuandika insha.

Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa mrejesho uliotolewa utawawezesha wadau mbalimbali wa elimu kuchukua hatua madhubuti za kuboresha ufundishaji na ujifunzaji na hivyo kuondoa changamoto zilizoainishwa katika taarifa hii. Endapo maoni yaliyotolewa yatafanyiwa kazi, ujuzi na maarifa watakayopata wanafunzi wa kidato cha pili katika somo hili utaongezeka na hatimaye kiwango cha ufaulu katika somo hili kitaongezeka. Baraza litashukuru kupokea maoni na mapendekezo kutoka kwa walimu na wadau wengine wa elimu kwa ujumla ambayo yatasaidia katika kuboresha taarifa ya uchambuzi wa maswali ya upimaji wa kidato cha pili. Baraza la Mitihani linapenda kutoa shukrani kwa maafisa mitihani, watahini, na wote waliohusika katika kuandaa taarifa hii.

Dkt. Charles E. Msonde
**KATIBU MTENDAJI**

# 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii inachambua kiwango cha kufaulu katika Upimaji wa Kidato cha Pili (FTNA) wa mwaka 2018, somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu. Upimaji huo uliofanyika mwezi Novemba 2018 uliandaliwa kwa kuzingatia muhtasari wa somo hili kwa kidato cha I na II.

Upimaji wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu ulikuwa na sehemu A, B na C na ulikuwa na jumla ya maswali saba yenye alama 100. Sehemu A ilikuwa na maswali mawili ambapo swali la kwanza lilikuwa la kuchagua jibu sahihi na swali la pili lilikuwa la kuoanisha maneno na sentensi. Sehemu hii ilikuwa na jumla ya alama 20 ambapo kila swali lilikuwa na alama 10. Sehemu B ilikuwa na maswali matatu ya kujaza majibu mafupi. Jumla ya alama katika sehemu hii ilikuwa 40 ambapo maswali mawili yalikuwa na alama 10 kila moja na swali moja lilikuwa na alama 20. Aidha, sehemu C ilikuwa na maswali mawili ambapo swali moja lilihitaji majibu mafupi na lingine lilikuwa la kuandika insha. Sehemu hii pia ilikuwa na alama 40 ambapo kila swali lilikuwa na alama 20.

Idadi ya wanafunzi walioandikishwa kufanya upimaji wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu mwaka 2018 ilikuwa 63,677 na waliofanya upimaji walikuwa 56,749. Hii ni sawa na ongezeko la zaidi ya wanafunzi 4,081 ukilinganisha na wanafunzi 52,668 waliofanya upimaji mwaka 2017. Aidha, wanafunzi 56,462 walipata matokeo ambapo wanafunzi 38,338 sawa na asilimia 67.90 walifaulu. Kati ya hawa, wanafunzi 802 (1.42%) walipata gredi A, 2064 (3.65%) walipata gredi B, 12,689 (22.47%) walipata gredi C na 22,783 (40.35%) walipata gredi D. Wanafunzi 18,124 sawa na asilimia 32.09 walifeli kwa kupata gredi F. Kwa ujumla kiwango cha kufaulu kwa mwaka 2018 kilikuwa asilimia 67.90, ongezeko la asilimia 1.84 ikilinganishwa na kiwango cha asilimia 66.06 kwa mwaka 2017.

Taarifa hii inaonesha uchambuzi wa maswali ya upimaji na majibu yaliyotolewa na wanafunzi. Sampuli za majibu ya wanafunzi zimewekwa ili kuonesha kile kilichofanywa na wanafunzi. Kufaulu kwa wanafunzi kwa mada kuligawanywa katika makundi matatu ambayo ni: vizuri, wastani na dhaifu. Kufaulu kwa mada kulikuwa dhaifu kama asilimia ya wanafunzi waliofanya vizuri ni 0 hadi 29; kufaulu kulikuwa wastani kama kulikuwa kati ya asilimia 30 hadi 64 na kufaulu kulikuwa kuzuri kati ya asilimia 65 hadi 100.

Hitimisho na mapendekezo kutokana na uchambuzi wa maswali ulivyofanyika imetolewa katika sehemu ya mwisho. Uchambuzi huu unatarajia kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu kwa wanafunzi na hatimaye kuwa na kiwango kizuri cha kufaulu kwa upimaji ujao.

## 2.0 TATHMINI YA KILA SWALI KWA MADA


## 2.1 SEHEMU A: SUNNAH NA HADITHI NA TAWHIID

Sehemu hii ilihusu mada za Sunnah na Hadithi na Tawhiid na ilkuwa na maswali mawili yenye jumla ya alama 20. Swali la kwanza lilikuwa la kuchagua jibu sahihi ambapo mwanafunzi alipewa sentensi yenye majibu manne (A, B, C na D) ya kuchagua na alitakiwa kuchagua herufi ya jibu moja sahihi na kujaza katika kisanduku. Swali la pili lilikuwa la kuoanisha maneno ambapo mwanafunzi alitakiwa aoanishe sentensi kumi zlizopo katika orodha A (i hadi x) na maneno yaliyopo katika orodha B (A hadi O) na kujaza katika visanduku alivyopewa chini ya swali.

### 2.1.1 Swali la 1: Sunnah na Hadithi-Uchaguzi wa Majibu Sahihi

Swali hili lilihusu mada ya *Sunnah na Hadithi* na lilikuwa na vipengele kumi (i-x) vilivyohusu mada ndogo za *Maana na Umuhimu wa Hadithi*, *Uandishi wa Hadithi za Mtume (s.a.w)*, *uchambuzi wa Hadithi za Mtume (s.a.w) na Hadithi za mafunzo maalum*. Mwanafunzi alitakiwa kuchagua jibu sahihi katika majibu manne aliyopewa (A - D) kisha aandike herufi ya jibu hilo katika kisanduku alichopewa. Swali hili lilikuwa na jumla ya alama 10 ambapo kila kipengele kati ya hivyo, kilikuwa na alama 1.

Wanafunzi 56,741 kati ya 56,749 waliofanya upimaji huu walijibu swali hili. Takwimu zinaonesha kuwa wanafunzi 419 (0.7%) walipata alama 0, wanafunzi 6,942 (16.1%) walipata alama 1 hadi 2 na wanafunzi 41,608 (73.3%) walipata alama 3 hadi 6. Wanafunzi waliopata alama 7 hadi 10 walikuwa 5,603 (9.9%) ambapo miongoni mwao wanafunzi 208 (0.4%) walipata alama zote 10. Chati ya 1 inaonesha kufaulu kwa wanafunzi kwa asilimia.




**Chati ya 1**: *Alama za Wanafunzi kwa Asilimia Katika Swali la 1*

Uchambuzi uliofanywa katika majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa kiwango cha kufaulu kwa wanafunzi katika swali hili kilikuwa kizuri ambapo wanafunzi 47,211 (83.2%) walipata alama kuanzia 3 hadi 10. Hata hivyo alama za wanafunzi hawa zilitofautiana kutokana na namna walivyochagua majibu. Vipengele vilivyojibiwa vizuri na wanafunzi hawa ni (i), (ii), (iv), (vi), (vii), (viii) (x) ambapo wanafunzi wengi waliweza kuchagua herufi za majibu sahihi. Wanafunzi 208 (0.4%) waliopata alama zote 10 za swali hili walikuwa na maarifa ya kutosha katika mada za Sunnah na Hadithi na pia walielewa matakwa ya swali. Hivyo, waliweza kuchagua majibu sahihi kwa vipengele vyote kumi vya swali hili. Kielelezo 1.1 kinaonesha mfano wa jibu la mwanafunzi aliyeweza kuchagua herufi za majibu sahihi kwa vipengele vyote kumi.

## Kielelezo 1.1

1. Katika kipengele (i) – (x), chagua jibu sahihi kisha **andika herufi yake** katika kisanduku.

(i) Neno "Sunnah" katika lugha ya kiarabu lina maana ya
   A mwenendo au mila.
   B jambo la ziada.
   C swala isiyo ya faradh.
   D kitendo cha kujipatia thawabu za ziada.

[A]

(ii) Katika elimu ya Hadithi, Matin ina maana ya
   A sehemu ya wasimulizi wa Hadithi.
   B mkusanyaji wa Hadithi.
   C maneno aliyoyasema Mtume (s.a.w) au maelezo ya swahaba kuhusu mtume.
   D maneno yanayohimiza au kukataza kufanya jambo.

[C]

(iii) Hadithi Nabawiyyi ni
   A habari aliyoitoa Mtume (s.a.w) kama alivyoipokea kutoka kwa Allah (s.w).
   B Hadithi isiyojulikana wasimulizi wake.
   C habari au usemi alioutoa Mtume (s.a.w) kwa maneno yake mwenyewe.
   D Hadithi dhaifu iliyosimuliwa na maswahaba.

[C]

(iv) Wakati wa Mtume (s.a.w) hapakuwa na uandishi mkubwa wa Hadithi kwa sababu
   A hakukuwa na waandishi.
   B Maswahaba walishughulika sana kuandika, kusoma na kuhifadh Qur'an.
   C Hakukuwa na wapokeaji mahiri wa Hadithi.
   D wanafiki waliwashawishi waislamu kutoandika Hadithi.

[B]

(v) Kazi kubwa ya kwanza ya uandishi wa Hadithi katika kipindi cha Maswahaba wa Mtume (s.a.w) ilifanywa na
   A Imam Malik    B Imam Shafi
   C Imam Muslim    D Sayyidina Ali

[D]

(vi) "Mtume (s.a.w) amesema Mwenye kutubia kabla jua halijachomoza upande wa magharibi, Allah atamkubalia toba yake". Miongoni mwa mafunzo yanayopatikana katika Hadithi hii ni
   A mwanadamu hana budi kuachana na maovu.
   B mwanadamu afanye toba ndani ya wakati wake sio wakati wa kufa au wakati wa dalili za wazi za kiama.
   C toba itakubaliwa na Allah (s.w) kama itafanywa usiku.
   D kila anayetubia Allah (s.w) humsamehe.

[B]

(vii) Kwa mujibu wa Hadithi ya Mtume (s.a.w) miongoni mwa njia za kujizuia na hasira ni kutamka
   A Ih-dina swiratal mustaqiim
   B Inna shwaitana kaana lakum aduwwah
   C Bismillah Rahman Rahim
   D Audhubillahi minashaitwaan Rajiim

[D]

(viii) Katika elimu ya Hadithi neno "Mutafakun alayhi" lina maana gani?
   A Hadithi inapatikana katika kitabu cha Bukhari na muslim.
   B Hadithi inayotumika kutolea ushahidi.
   C Hadithi iliyoandikwa tokea wakati wa Mtume (s.a.w).
   D Hadithi iliyoandikwa wakati wa maswahaba.

[A]

(ix) Al-muwatta ni kitabu cha Hadithi kilichoandikwa wakati wa
   A uhai wa Mtume (s.a.w).
   B Maswahaba wa Mtume (s.a.w)
   C wafuasi wa wafuasi wa maswahaba (Tabii Tubiina).
   D wafuasi wa Maswahaba (Tabiina).

[D]

(x) "Kuipenda nchi yako ni katika imani". Hadithi hii ni mfano wa Hadithi gani?
   A Hassan    B Maudhui
   C Dhaifu    D Sahihi

[B]

Kielelezo 1.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyechagua herufi za majibu sahihi kwa vipengele vyote kumi vya swali.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa wanafunzi 41,608 walipata alama za wastani (3 hadi 6) kwa sababu walichagua majibu sahihi katika vipengele visivyozidi sita kati ya kumi vya swali hili. Kwa upande mwingine, wanafunzi 9,530 (16.8%) walipata alama za chini (0 hadi 2) kwa kuwa hawakuwa na maarifa ya kutosha ya mada ya Sunnah na Hadithi. Vipengele ambavyo havikujibiwa kwa usahihi na wanafunzi wengi ni kipengele cha (i), (iii) na (ix).

Katika kipengele (i) kinachohusu maana ya neno Sunnah katika lugha ya kiarabu, wanafunzi wengi walichagua D (kitendo cha kujipatia thawabu za ziada) badala ya A (mwenendo au mila) ambalo likuwa jibu sahihi. Pia baadhi ya wanafunzi walichagua B (jambo la ziada) kutokana na kueleweka vibaya kwa maana ya Sunnah na hivyo kufikiria kuwa ni kitu cha ziada kama inavyotafsiriwa kimakosa na baadhi ya Waislamu kuwa Sunnah ni matendo yasiyo ya lazima ambayo ukiyatenda utapata thawabu na ukiyaacha hupati dhambi badala ya mwenendo au mila.

Katika kipengele cha (iii) kilichouliza maana ya Hadithi Nabawiyyi wanafunzi hawa pia walichagua A (habari aliyoitoa Mtume (s.a.w) kama alivyoipokea kutoka kwa Allah (s.w), badala ya C (habari au usemi alioutoa Mtume (s.a.w) kwa maneno yake mwenyewe). Wanafunzi hawa wamechanganya maana ya Hadithi Nabawiyyi na Qudusi. Hii ilisababisha wanafunzi hawa kuchagua jibu la A badala ya jibu sahihi la B.

Vilevile katika kipengle cha (ix) kinachouliza kipindi kilichoandikwa kitabu cha Hadithi Al-muwatta, wanafunzi wengi walichagua C (kipindi cha wafuasi wa wafuasi wa Maswahaba, Tabii Tabiina) badala ya D (wakati wa wafuasi wa Maswahaba, Tabiina) ambalo lilikuwa ndiyo jibu sahihi. Ingawa wanafunzi wengi wanajua kuwa kipindi cha Mtume (s.a.w) Hadithi hazikuandikwa hivyo hawakuchagua A lakini walishindwa kutofautisha vipindi viwili vya wafuasi wa wafuasi wa maswahaba (Tabii Tabiina) na wafuasi wa Maswahaba (Tabiina) na hivyo wengi wao walichagua jibu ambalo sio sahihi la C. Wanafunzi wachache walichagua B (wakati wa Maswahaba) kutokana na kutokuwa na maarifa ya Mada ya Sunnah na Hadithi.

Kwa upande mwingine, kulikuwa na wanafunzi 419 ambao hawakuwa na maarifa ya mada za Sunnah na Hadithi hivyo waliandika herufi za majibu ambayo sio sahihi katika vipengele vyote 10 na hivyo kupata alama 0.

Kielelezo 1.2 kinaonesha mfano wa jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kuchagua majibu sahihi katika vipengele vyote kumi.

**Kielelezo 1.2**

1. Katika kipengele (i) – (x), chagua jibu sahihi kisha **andika herufi yake** katika kisanduku.

(i) Neno "Sunnah" katika lugha ya kiarabu lina maana ya
A mwenendo au mila.
B jambo la ziada.
C swala isiyo ya faradh.
D kitendo cha kujipatia thawabu za ziada.

B

(ii) Katika elimu ya Hadithi, Matin ina maana ya
A sehemu ya wasimulizi wa Hadithi.
B mkusanyaji wa Hadithi.
C maneno aliyoyasema Mtume (s.a.w) au maelezo ya swahaba kuhusu mtume.
D maneno yanayohimiza au kukataza kufanya jambo.

A

(iii) Hadithi Nabawiyyi ni
A habari aliyoitoa Mtume (s.a.w) kama alivyoipokea kutoka kwa Allah (s.w).
B Hadithi isiyojulikana wasimulizi wake.
C habari au usemi alioutoa Mtume (s.a.w) kwa maneno yake mwenyewe.
D Hadithi dhaifu iliyosimuliwa na maswahaba.

D

(iv) Wakati wa Mtume (s.a.w) hapakuwa na uandishi mkubwa wa Hadithi kwa sababu
A hakukuwa na waandishi.
B Maswahaba walishughulika sana kuandika, kusoma na kuhifadh Qur'an.
C Hakukuwa na wapokeaji mahiri wa Hadithi.
D wanafiki waliwashawishi waislamu kutoandika Hadithi.

A

(v) Kazi kubwa ya kwanza ya uandishi wa Hadithi katika kipindi cha Maswahaba wa Mtume (s.a.w) ilifanywa na
A Imam Malik   B Imam Shafi
C Imam Muslim   D Sayyidina Ali

A

(vi) "Mtume (s.a.w) amesema Mwenye kutubia kabla jua halijachomoza upande wa magharibi, Allah atamkubalia toba yake". Miongoni mwa mafunzo yanayopatikana katika Hadithi hii ni
A mwanadamu hana budi kuachana na maovu.
B mwanadamu afanye toba ndani ya wakati wake sio wakati wa kufa au wakati wa dalili za wazi za kiama.
C toba itakubaliwa na Allah (s.w) kama itafanywa usiku.
D kila anayetubia Allah (s.w) humsamehe.

D

(vii) Kwa mujibu wa Hadithi ya Mtume (s.a.w) miongoni mwa njia za kujizuia na hasira ni kutamka
A Ih-dina swiratal mustaqiim
B Inna shwaitana kaana lakum aduwwah
C Bismillah Rahman Rahim
D Audhubillahi minashaitwaan Rajiim

B

(viii) Katika elimu ya Hadithi neno "Mutafakun alayhi" lina maana gani?
A Hadithi inapatikana katika kitabu cha Bukhari na muslim.
B Hadithi inayotumika kutolea ushahidi.
C Hadithi iliyoandikwa tokea wakati wa Mtume (s.a.w).
D Hadithi iliyoandikwa wakati wa maswahaba.

C

(ix) Al-muwatta ni kitabu cha Hadithi kilichoandikwa wakati wa
A uhai wa Mtume (s.a.w).
B Maswahaba wa Mtume (s.a.w)
C wafuasi wa wafuasi wa maswahaba (Tabii Tubiina).
D wafuasi wa Maswahaba (Tabiina).

B

(x) "Kuipenda nchi yako ni katika imani". Hadithi hii ni mfano wa Hadithi gani?
A Hassan B Maudhui
C Dhaifu D Sahihi

A


Kielelezo 1.2 kinaonesha mfano wa jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kuchagua majibu sahihi katika vipengele vyote kumi.

### 2.1.2 Swali la 2: Tawhiid - Kuoanisha Maneno na Sentensi

Swali hili lilihusu mada za Tawhiid katika dhana ya dini. Mwanafunzi alitakiwa kuoanisha vipengele vya maneno kumi na tano (A - O) kutoka orodha B na sentensi kumi (i-x) kutoka orodha A kisha kujaza herufi yake katika jedwali alilopewa. Swali lilikuwa na vipengele kumi (i) - (x) ambapo vipengele (i) - (ii) vilihusu mtu anayekanusha kiutendaji maamrisho ya Allah na mtu anayemnyenyekea Allah (sw) na kufuata sheria zake. Kipengele cha (iii) kilihusu mfumo wa maisha wenye kujisalimisha kwa Allah. Kipengele (iv) kilihusu mfumo wa maisha wa kujitenga na harakati za maendeleo ya mwanadamu hapa ulimwenguni. Kipengele cha (v) kilihusu njia ya maisha anayoifuata mwanadamu katika maisha yake ya kila siku. Kipengele cha (vi) kilihusu mfumo wa maisha ambao wafuasi wake

wameacha muongozo wa Allah (s.w) kupitia Taurati. Kipengle cha (vii) kilihusu mfumo wa maisha ambao wafuasi wake humnasibisha mtume wao kama mwana wa mungu. Kipengle cha (viii) kilihusu mfumo wa maisha unaojinasibisha na kutokuwa na imani ya dini kabisa. Ili hali kipengle cha (ix) kilihusu mfumo wa maisha ambao wafuasi wake hunasibishwa na kabila au rangi na Kipengele cha (x) kilihusu mfumo wa maisha ambao wafuasi wake wanakanusha kiutendaji maamrisho ya Allah (s.w). Swali hili lilikuwa na alama 10 ambapo kila kipengele kilikuwa na alama 1.

Wanafunzi 56,719 kati ya 56,749 waliofanya upimaji huu walijibu swali hili. Takwimu zinaonesha kuwa wanafunzi 1,093 (1.9%) walipata alama 0, wanafunzi 6,942 (12.2%) walipata alama 1 hadi 2, wanafunzi 33,059 (58.3%) walipata alama 3 hadi 6. Wanafunzi waliopata alama 7 hadi 10 walikuwa ni 15,625 (27.5%) na miongoni mwao wanafunzi 863 (1.5%) walipata alama zote 10. Chati 2 inaonesha kufaulu kwa wanafunzi kwa asilimia.




**Chati ya 2**: *Alama za Wanafunzi kwa Asilimia Katika Swali la 2*

Uchambuzi uliofanywa katika majibu ya wanafunzi ulionesha kuwa, kiwango cha kufaulu kwa wanafunzi katika swali hili ni kizuri. Wanafunzi 48,684 (85.8%) walipata alama 3 hadi 10 ambazo zilikuwa alama za kufaulu kwenye swali hili. Vipengele vilivyooanishwa kwa usahihi na

wanafunzi wengi ni; (i), (ii), (iii), (v), (vii), (viii) na (x). Wanafunzi 863 (1.5%) waliopata alama zote 10 walielewa matakwa ya swali na walikuwa na maarifa ya kutosha ya mada za Tawhiid yaliyowawezesha kuoanisha kwa usahihi vipengele vyote vya swali hili. Kielelezo 2.1 kinaonesha mfano wa jibu la mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi vipengele vyote 10.

**Kielelezo 2.1**

2. Oanisha maneno kutoka **Orodha B** na sentensi kutoka **Orodha A** kisha jaza herufi yake katika jedwali.

| **Orodha A** | **Orodha B** |
|---|---|
| (i) Mtu anayekanusha kiutendaji maamrisho ya Allah (s.w) yaliyobainishwa wazi katika vitabu vyake na mitume yake. | A Utawa<br>B Ukristo |
| (ii) Mtu anayemnyenyekea Allah (s.w) kwa kufuata kwa ukamilifu sheria zake zote. | C Ushirikina<br>D Uyahudi |
| (iii) Mfumo wa maisha unaoendeshwa kwa kujisalimisha kwa Allah (s.w) katika kila kipengele cha maisha. | E Kafiri<br>F Uhafidhina |
| (iv) Mfumo wa maisha ambao wafuasi wake hujitenga mbali na harakati za maendeleo ya mwanadamu hapa ulimwenguni. | G Uhindu<br>H Uislamu |
| (v) Mfumo au njia ya maisha anayoifuata mwanadamu katika maisha yake ya kila siku. | I Muislamu<br>J Ukafiri |
| (vi) Mfumo wa maisha ambao wafuasi wake wameacha muongozo wa Allah (s.w) kupitia Taurati na kufuata wanazuoni wao. | K Ibada<br>L Upagani |
| (vii) Mfumo wa maisha ambao wafuasi wake humnasibisha mtume wao kama mwana wa mungu. | M Dini<br>N Udini |
| (viii) Mfumo wa maisha unaojinasibisha na kutokuwa na imani ya dini kabisa. | O Ubudha |
| (ix) Mfumo wa maisha ambao wafuasi wake hunasibishwa na kabila au rangi. | |
| (x) Mfumo wa maisha ambao wafuasi wake wanakanusha kiutendaji maamrisho ya Allah (s.w) yaliyobainishwa wazi katika vitabu vyake na mitume yake. | |

| **Orodha A** | (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) | (vi) | (vii) | (viii) | (ix) | (x) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Orodha B** | E | I | H | A | M | D | B | L | G | J |

Kielelezo 2.1 kinaonesha mfano wa jibu la mwanafunzi aliyeweza kuoanisha kwa usahihi vipengele vyote (i – x).

Kwa upande mwingine, wanafunzi 33,059 (58.3%) walipata alama za wastani kwa sababu waliweza kuoanisha kwa usahihi baadhi ya vipengele vya swali hili kutokana na kuwa na maarifa madogo katika mada ya Tawhiid hivyo walipata chini ya alama 7. Vipengele ambavyo havikuwa vimeoanishwa kwa usahihi kwa baadhi ya wanafunzi hawa ni (iv), (vi) na (ix).

Katika kipengele cha (iv) kilichohusu mfumo wa maisha ambao wafuasi wake hujitenga mbali na harakati za maendeleo ya mwanadamu hapa ulimwenguni, wanafunzi wengi walijaza C (ushirikina) badala ya A (Utawa) kutokana na kutokuwa na maarifa ya kutosha. Sababu kubwa ya wanafunzi kushindwa kuchagua jibu sahihi katika kipengele hiki ni kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dini mbalimbali zilizopo duniani na itikadi za dini hizo. Wanafunzi wengi wamezoea kusikia neno ushirikina katika masiko yao ndio maana baada ya kushindwa kujua jibu sahihi wakakimbilia kwa wingi kuchagua ushirikina badala ya utawa.

Katika kipengele cha (vi) kilichohusu mfumo wa maisha ambao wafuasi wake wameacha muongozo wa Allah (s.w) kupitia Taurati na kufuata wanazuoni wao, wanafunzi wengi walijaza J (ukafiri) badala ya D (Uyahudi) kwa vile walikosa maarifa ya kutosha kuhusu mifumo mbalimbali ya maisha kama ilivyofafanuliwa katika Uislamu.

Katika kipengele cha (ix) kilichohusu mfumo wa maisha ambao wafuasi wake hunasibishwa na kabila au rangi, wanafunzi wengi walijaza F (Uhafidhina) badala ya G (Uhindu) kutokana na kutokuwa na elimu ya kutosha kuhusiana na dini au mifumo mbalimbali ya maisha iliyopo duniani.

Uchambuzi zaidi umeonesha kuwa wanafunzi 1,093 (1.9%) walipata alama 0 kwa sababu walishindwa kuoanisha vipengele vyote vya swali hili kutokana na kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada za Tawhid. Kielelezo 2.2 kinaonesha mfano wa jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kuoanisha kwa usahihi vipengele vyote 10 vya swali.

## Kielelezo 2.2

2. Oanisha maneno kutoka **Orodha B** na sentensi kutoka **Orodha A** kisha jaza herufi yake katika jedwali.

| **Orodha A** | | **Orodha B** | |
|---|---|---|---|
| (i) | Mtu anayekanusha kiutendaji maamrisho ya Allah (s.w) yaliyobainishwa wazi katika vitabu vyake na mitume yake. | A | Utawa |
| | | B | Ukristo |
| (ii) | Mtu anayemnyenyekea Allah (s.w) kwa kufuata kwa ukamilifu sheria zake zote. | C | Ushirikina |
| | | D | Uyahudi |
| (iii) | Mfumo wa maisha unaoendeshwa kwa kujisalimisha kwa Allah (s.w) katika kila kipengele cha maisha. | E | Kafiri |
| | | F | Uhafidhina |
| (iv) | Mfumo wa maisha ambao wafuasi wake hujitenga mbali na harakati za maendeleo ya mwanadamu hapa ulimwenguni. | G | Uhindu |
| | | H | Uislamu |
| (v) | Mfumo au njia ya maisha anayoifuata mwanadamu katika maisha yake ya kila siku. | I | Muislamu |
| | | J | Ukafiri |
| (vi) | Mfumo wa maisha ambao wafuasi wake wameacha muongozo wa Allah (s.w) kupitia Taurati na kufuata wanazuoni wao. | K | Ibada |
| | | L | Upagani |
| (vii) | Mfumo wa maisha ambao wafuasi wake humnasibisha mtume wao kama mwana wa mungu. | M | Dini |
| | | N | Udini |
| (viii) | Mfumo wa maisha unaojinasibisha na kutokuwa na imani ya dini kabisa. | O | Ubudha |
| (ix) | Mfumo wa maisha ambao wafuasi wake hunasibishwa na kabila au rangi. | | |
| (x) | Mfumo wa maisha ambao wafuasi wake wanakanusha kiutendaji maamrisho ya Allah (s.w) yaliyobainishwa wazi katika vitabu vyake na mitume yake. | | |

| **Orodha A** | (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) | (vi) | (vii) | (viii) | (ix) | (x) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Orodha B** | M | N | G | C | H | F | D | E | A | K |

Kielelezo 2.2 kinaonesha mfano wa jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kuoanisha kwa usahihi vipengele vyote (i) – (x).


## 2.2 SEHEMU B: TAWHID, TAREKH NA QUR'AN

Sehemu hii ilihusu mada za Tawhiid, Tarekh na Qur'an na ilikuwa na maswali matatu yenye jumla ya alama 40. Swali la tatu lilikuwa na sentensi kumi ambapo mwanafunzi alitakiwa kuandika kweli au si kweli kwa kila sentensi. Swali la nne ni la kujaza nafasi zilizowazi ambapo mwanafunzi alitakiwa kuchagua neno sahihi kutoka katika jedwali na kulijaza ili kukamilisha sentensi. Swali la tano lilikuwa na vipengele viwili (a) na (b) na lilimtaka mwanafunzi kupanga nukuu tano alizopewa kwa mpangilio sahihi ili zilete mantiki.

### 2.2.1 Swali la 3: Tawhiid - Kujibu Kweli au si Kweli

Swali hili lilihusu mada za Tawhiid na lilimtaka mwanafunzi aandike "Kweli" kwenye sentensi ambayo ni sahihi, na "Si Kweli" kwenye sentensi ambayo si sahihi. Swali lilikuwa na vipengele 10 (i) - (x) vilivyojumuisha mada za Tawhiid za (i) Dhana ya Imani katika Uislamu; (ii), (iii), (iv), (vi) nguzo za Imani; (v), (vii), (viii) (ix) na (x) inahusu dhana ya Dini kwa mujibu wa Qur'an.

Wanafunzi 56,745 kati ya 56,749 waliofanya upimaji huu walijibu swali hili. Takwimu zinaonesha kuwa wanafunzi 70 (0.1%) walipata alama 0, wanafunzi 998 (1.8%) walipata alama 1 hadi 2 na wanafunzi 27,033 (47.6%) walipata alama 3 hadi 6. Wanafunzi waliopata alama 7 hadi 10 ni 28,644 (50.5%) na miongoni mwao wanafunzi 1,242 (2.2%) walipata alama zote 10. Chati ya 3 inaonesha kufaulu kwa wanafunzi kwa asilimia.




**Chati ya 3:** *Alama za Wanafunzi kwa Asilimia Katika Swali la 3*

Kwa ujumla kiwango cha kufaulu kwa wanafunzi katika swali hili ni kizuri sana kwa kuwa wanafunzi 55,677 (98.1%) walipata alama 3 hadi 10 ambazo zilikuwa alama za kufaulu kwa swali hili. Wanafunzi hawa waliweza kujibu kwa usahihi vipengele zaidi ya saba kwa kuandika kweli au si kweli. Vipengele ambavyo vimejibiwa vizuri na wanafunzi wengi ni cha (i) kilichohusu Tawhiid ambayo ni fani inayohusiana na Imani ya kumpwekesha Allah (s.w) na cha (ii) kinachohusu Nguzo za Imani ya

kiislamu ambazo ni tano, cha (iii) kinachusu Zaburi ambacho ni kitabu alichoteremshiwa Nabii Issa (a.s), cha (v) kinachohusu Ukristo ni miongoni mwa dini zinazompwekesha Allah (s.w), na vipengele vya (vi), (ix) vinavyohusu kuamini qadar ni miongoni mwa nguzo za imani na cha (x) kinachohusu Dini za watu ambayo ni mifumo ya maisha iliyowekwa na wanadamu kwa kuzingatia muongozo wa Allah (s.w). Wanafunzi 1,242 (2.2%) waliopata alama zote 10 walielewa matakwa ya swali, na walikuwa na maarifa ya kutosha ya mada za Tawhiid yaliyowawezesha kujibu vipengele vyote kwa usahihi. Kielelezo 3.1 kinaonesha mfano wa jibu la mwanafunzi aliyejibu kwa kufuata maelekezo ya swali.

**Kielelezo 3.1**

3. Andika **Kweli** kama sentensi ni sahihi au **Si Kweli** ikiwa sentensi si sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi.

(i) Tawhiid ni fani inayohusiana na imani ya kumpwekesha Allah (s.w) ……Kweli……

(ii) Nguzo za imani ya kiislamu ni tano……Si Kweli……

(iii) Zaburi ni kitabu alichoteremshiwa Nabii Issa (a.s) ……Si Kweli……

(iv) Taurat, Zabur na Injili ni vitabu walivyovikuta Waislamu vikiwa mikononi mwa Mayahudi na Wakristo……Kweli……

(v) Ukristo ni miongoni mwa dini zinazompwekesha Allah (s.w) ……Si Kweli……

(vi) Kuamini Qadar ni miongoni mwa nguzo za imani ……Kweli……

(vii) Kwa mtazamo wa Uislamu dini ni imani inayohusiana na mambo ya kiroho baina ya binadamu na Mwenyezi Mungu tu ……Si Kweli……

(viii) Katika lugha ya kiarabu siku ya malipo ni miongoni mwa maana ya dini ……Kweli……

(ix) Ushirikina nao ni dini au mfumo wa maisha unaowaongoza washirikina katika maisha yao kila siku ……Kweli……

(x) Dini za watu ni mifumo ya maisha iliyowekwa na wanadamu kwa kuzingatia muongozo wa Allah (s.w) ……Si Kweli……

Kielelezo 3.1 kinaonesha mfano wa jibu la mwanafunzi aliyepata alama zote 10. Aliweza kutambua sentensi sahihi ambazo aliandika kweli, na sentensi zisizo sahihi ambazo aliandika si kweli.

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa wanafunzi 27,033 (47.6%) waliopata alama za wastani hawakuwa na maarifa ya kutosha ya mada za Tawhiid na walipata baadhi ya vipengele tu. Vipengele

vilivyokosewa sana na wanafunzi hawa ni cha (iv) na cha (viii). Kipengele cha (iv) kilichohusu vitabu vya Taurat, Zabur na Injili walivyovikuta Waislamu vikiwa mikononi mwa Mayahudi na Wakristo, wanafunzi hawa walijibu sio kweli wakati jibu sahihi ni kweli. Wanafunzi hawakuwa na ufahamu wa historia ya vitabu vilivyoshuhswa na Mwenyezi Mungu pamoja na jamii zilizoshushiwa vitabu hivyo. Kipengele cha (viii) kilichohusu maana ya neno dini katika lugha ya kiarabu kuwa na maana ya siku ya malipo, wanafunzi hawa walijibu sio kweli wakati jibu sahihi lilikuwa ni kweli. Vilevile kulikuwa na wanafunzi 70 (1.9%) waliopata alama 0 kwa sababu walikosa vipengele vyote 10 vya swali hili. Wanafunzi hawa walikuwa na uelewa mdogo wa mada ya Tawhiid na hivyo walishindwa kutofautisha sentensi za kweli na ambazo sio za kweli. Kwa mfano, katika kipengele cha (viii) ambacho wanafunzi wengi walijibu si kweli wakati jibu sahihi ni kweli, wanafunzi hawa walionekana kutokuwa na ufahamu wa kitabu cha Qur’an ambacho kuna aya mbalimbali zinazozungumzia siku ya malipo ikihusihswa na maana ya dini. Pia wanafunzi walihitaji kuwa na kiasi kidogo cha ufahamu wa lugha ya kiarabu lakini wanafunzi hawa hawakuwa nao. Kielelezo 3.2 kinaonesha mfano wa jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kujua sentensi za kweli na ambazo si za kweli.

## Kielelezo 3.2

3. Andika **Kweli** kama sentensi ni sahihi au **Si Kweli** ikiwa sentensi si sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi.

(i) Tawhiid ni fani inayohusiana na imani ya kumpwekesha Allah (s.w) ……Si kweli……

(ii) Nguzo za imani ya kiislamu ni tano……Kweli……

(iii) Zaburi ni kitabu alichoteremshiwa Nabii Issa (a.s) ……kweli……

(iv) Taurat, Zabur na Injili ni vitabu walivyovikuta Waislamu vikiwa mikononi mwa Mayahudi na Wakristo……Si kweli……

(v) Ukristo ni miongoni mwa dini zinazompwekesha Allah (s.w) ……Kweli……

(vi) Kuamini Qadar ni miongoni mwa nguzo za imani ……Si kweli……

(vii) Kwa mtazamo wa Uislamu dini ni imani inayohusiana na mambo ya kiroho baina ya binadamu na Mwenyezi Mungu tu ……Kweli……

(viii) Katika lugha ya kiarabu siku ya malipo ni miongoni mwa maana ya dini ……Si kweli……

(ix) Ushirikina nao ni dini au mfumo wa maisha unaowaongoza washirikina katika maisha yao kila siku ……Si kweli……


(x) Dini za watu ni mifumo ya maisha iliyowekwa na wanadamu kwa kuzingatia muongozo wa Allah (s.w) ……kweli……

Kielelezo 3.2 kinaonesha mfano wa jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kujaza jibu sahihi kwa sentensi zote 10.

### 2.2.2 Swali la 4: Tarekh - Kujaza Nafasi Zilizowazi

Swali hili lilihusu mada za Tarekh ambazo zilijumuisha vipengele (a), (b), (c) na (d) vilivyohusu Dhana juu ya Historia; vipengele (e), (f) na (g) vilivyohusu Historia ya Mitume walioteuliwa; na vipengele (h) (i) na (j) vilivyohusu Bara la Arab Zama za Jahiliya. Swali lilikuwa na vipengele 10 na lilimtaka mwanafunzi ajaze nafasi zilizoachwa wazi katika kipengele (a) hadi (j) kwa kutumia maneno aliyopewa kwenye jedwali. Swali lilikuwa na jumla ya alama 10 na kila kipengele kilikuwa na alama 1.

Wanafunzi 56,721 kati ya 56,749 waliofanya upimaji huu walijibu swali hili. Takwimu zinaonesha kuwa wanafunzi 2,739 (4.8) walipata alama 0, wanafunzi 14,805 (26%) walipata alama 1 hadi 2 na wanafunzi 33,053 (58.3%) walipata alama 3 hadi 6. Wanafunzi waliopata alama 7 hadi 10 walikuwa 6,124 (10.8%) na miongoni mwao wanafunzi 39 (0.2%) walipata alama zote 10. Chati ya 4 inaonesha kufaulu kwa wanafunzi kwa asilimia.




**Chati ya 4**: *Alama za Wanafunzi kwa Asilimia Katika Swali la 4*

Kwa ujumla kiwango cha kufaulu kwa wanafunzi katika swali hili ni kizuri kwani wanafunzi 39,177 (69.1%) waliojibu swali hili walipata alama 3 hadi 10 ambazo zilikuwa alama za kufaulu kwa swali hili. Wanafunzi hawa waliweza kujibu kwa usahihi vipengele zaidi ya saba. Vipengele ambavyo vimejibiwa vizuri na wanafunzi wengi ni; (a), (b), (c) (g), (h), (i) na (j). Hata hivyo alama za wanafunzi kwenye swali hili zilitofautiana kutokana na kukosa baadhi ya vipengele. Wanafunzi 39 ndio waliweza kupata alama zote 10 za swali hili. Wanafunzi hawa walikuwa na maarifa ya

kutosha ya mada za Tarekh na pia walielewa matakwa ya swali hivyo waliweza kuchagua majibu sahihi kutoka katika jedwali kwenye vipengele vyote 10. Kielelezo 3.1 kinaonesha mfano wa jibu la mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi na kufuata maelekezo ya swali.

**Kielelezo 4.1**

4. Kwa kutumia maneno uliyopewa, chagua jibu sahihi ili kujaza nafasi wazi katika vipengele (a) – (j)

Al-qaaba, Darwin, Nabii Muhammad (s.a.w), Nabii Nuhu (a.s), mada, nyani, Jahiliyah, Mfalme Najash, Mfalme Nimrudi, Nabii Ibrahim (a.s), Allah (s.w), Khalifa, Nabii Mussa (a.s), shamu, Karl Marx

(a) Mtazamo wa makafiri juu ya chanzo cha ulimwengu, mwanadamu na vitu vyote kwa ujumla ni ....mada..................

(b) Mwanzilishi wa itikadi ya kijamaa na chimbuko la ukafiri wa kumkana Mwenyezi Mungu anaitwa ...Karl Marx............

(c) Kiongozi anayeutawala ulimwengu kwa kufuata mwongozo wa Allah (s.w) anajulikana jina la ........Khalifa..........

(d) Uzushi juu ya chimbuko na asili ya mwanadamu unaonesha kuwa ulitokana na ...Darwin..............

(e) Mlinganiaji Uislamu katika mazingira magumu bila ya kukata tamaa kwa muda wa miaka 950 anaitwa .....Nabii Nuh a.s

(f) Kiongozi aliyekabiliana na Nabii Ibrahim (a.s) na kujipa uungu kama ilivyokuwa kwa Firaun ni .....Mfalme Nimrudi

(g) Mtume aliyeandaliwa na Allah (s.w) kuwakomboa Bani Israil alikuwa ...Nabii Musa a.s.

(h) Zama ambazo watu wa Bara Arab na kwingineko duniani walikuwa katika kiza ni ......Jahiliyah...

(i) Moja kati ya alama inayoonesha utukufu wa mji wa Makkah ulimwenguni ni ...Al-qaaba

(j) Miongoni mwa mji maarufu kwa misafara ya biashara uarabuni ni ....Shamu...............

Kielelezo 4.1 kinaonesha mfano wa jibu la mwanafunzi aliyeweza kuchagua majibu sahihi kutoka katika jedwali na kujaza inavyotakiwa katika vipengle vyote 10.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa wanafunzi 33,053 (58.3%) kati ya 56,721 waliojibu swali, walipata alama za wastani (3 hadi 6) kwa sababu walimudu kujaza majibu sahihi kwa baadhi ya vipengele. Wanafunzi hawa walikuwa wanaelewa mada za Tarekh kwa kiasi fulani. Wanafunzi 17,544 (30.9%) walipata alama za chini (0 hadi 2) kwa sababu hawakuwa na maarifa ya mada za Tarekh. Wanafunzi hawa walichanganya baadhi ya majina ya watu na matukio yaliyomo kwenye vipengele (a) - (j). Kutokana na dosari hiyo, walijaza majibu yasiyo sahihi. Vipengele ambavyo wanafunzi walishindwa kujibu kwa usahihi ni; (d), (e) na (f).

Katika kipengele (d) wanafunzi walishindwa kujaza jina la mwanasayansi Darwin aliyeandika uzushi juu ya chimbuko la asili ya mwanadamu. Wanafunzi hawa hawakuwa na maarifa ya kutosha ya mada ya Tarekh, kwa kuchanganya mtazamo wa makafiri juu ya chanzo cha mwanadamu ambapo wengi wao walijibu Nyani badala ya Darwin ambaye ndiye muanzilishi wa nadharia hiyo. Wanafunzi hawa walitumia nadharia ya historia katika kujibu kipengele hiki, badala ya historia ya Uislamu.

Katika kipengele (e) wanafunzi waliulizwa mlinganiaji Uislamu katika mazingira magumu bila ya kukata tamaa kwa muda wa miaka 950 ambapo walijibu Nabii Ibrahimu badala ya Nabii Nuhu ambalo ndio jibu sahihi. Baadhi ya wanafunzi walichagua majibu mengine ambayo pia hayakuwa sahihi kama vile Nabii Musa (a.s), Muhammad (s.a.w), Khalifa, Alqaaba na Karl Marx. Kwa jumla wanafunzi hawa hawakuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu historia ya maisha ya Nabii Nuhu (a.s) na hivyo wakaamua kujibu kwa kubahatisha. Wanafunzi wengine walikimbilia kuchagua Nabii Ibrahim baada ya kuwa hawajui jibu na kwa kuwa Nabii huyu ni maarufu wakaamua wamchague kama jibu sahihi.

Katika kipengele (f) wanafunzi waliulizwa jina la kiongozi aliyekabiliana na Nabii Ibrahim (a.s) na kujipa uungu kama ilivyokuwa kwa Firauni ambapo wengi walijaza Najash badala ya Namrud ambalo ndilo jibu sahihi. Sababu kubwa ya wanafunzi hawa kushindwa kipengele hiki ni kutokana na kutokuwa na maarifa ya kutosha juu ya historia ya nabii Ibrahim na Namrud. Katika Uislamu Historia hii ya Namrud kuhusishwa na uungu haina umaarufu sana kama ya Firauni na ndio sababu wanafunzi wengi walichagua Najash ambaye ni maarufu katika historia ya Uislamu ingawa hajawahi kujiita Mungu. Kielelezo 4.2 kinaonesha mfano wa jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi vipengele (a) – (j).

**Kielelezo 4.2**

4. Kwa kutumia maneno uliyopewa, chagua jibu sahihi ili kujaza nafasi wazi katika vipengele (a) – (j)

| |
|---|
| Al-qaaba, Darwin, Nabii Muhammad (s.a.w), Nabii Nuhu (a.s), mada, nyani, Jahiliyah, Mfalme Najash, Mfalme Nimrudi, Nabii Ibrahim (a.s), Allah (s.w), Khalifa, Nabii Mussa (a.s), shamu, Karl Marx |

(a) Mtazamo wa makafiri juu ya chanzo cha ulimwengu, mwanadamu na vitu vyote kwa ujumla ni ..Jahiliyah............

(b) Mwanzilishi wa itikadi ya kijamaa na chimbuko la ukafiri wa kumkana Mwenyezi Mungu anaitwa ..~~Jahiliyah~~..mada

(c) Kiongozi anayeutawala ulimwengu kwa kufuata mwongozo wa Allah (s.w) anajulikana jina la ..Nabii..Muhammad (s.a.w)

(d) Uzushi juu ya chimbuko na asili ya mwanadamu unaonesha kuwa ulitokana na ...Nyani...............

(e) Mlinganiaji Uislamu katika mazingira magumu bila ya kukata tamaa kwa muda wa miaka 950 anaitwa ..Nabii...Ibrahim...(a.s)

(f) Kiongozi aliyekabiliana na Nabii Ibrahim (a.s) na kujipa uungu kama ilivyokuwa kwa Firaun ni ..Mfalme..Najash

(g) Mtume aliyeandaliwa na Allah (s.w) kuwakomboa Bani Israil alikuwa ..Nabii..Nuhu (a.s)

(h) Zama ambazo watu wa Bara Arab na kwingineko duniani walikuwa katika kiza ni ...Darwin........

(i) Moja kati ya alama inayoonesha utukufu wa mji wa Makkah ulimwenguni ni .Shamu....


(j) Miongoni mwa mji maarufu kwa misafara ya biashara uarabuni ni .Karl...Marx........

Kielelezo 4.2 kinaonesha mfano wa jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kichagua majibu sahihi kutoka katika jedwali kwa vipengele vyote 10.

### 2.2.3 Swali la 5: Qur'an - Kupanga Nukuu Katika Mpangilio sahihi

Swali hili lilihusu mada ya Qur'an na lilikuwa na vipengele viwili (a) na (b). Kipengele (a) kilihusu kushuka na kuhifadhiwa kwa Qur'an na kipengele (b) kilihusu kusoma na kuhifadhi Sura zilizoteuliwa. Katika kila kipengele mwanafunzi alitakiwa kupanga nukuu katika mtiririko unaotakiwa ili kupata maana iliyokamilika. Swali lilikuwa na jumla ya alama 20 ambapo kila kipengele kilikuwa na alama 10.

Wanafunzi 56,708 kati ya 56,749 waliofanya upimaji walijibu swali hili. Takwimu zinaonesha kuwa wanafunzi 6299 (11.1%) walipata alama 0, wanafunzi 21,437 (37.8%) walipata alama 1 hadi 5.5 na wanafunzi 24,066 (42.4%) walipata alama 6 hadi 12. Wanafunzi waliopata alama 13 hadi 20 walikuwa 4905 (8.6%) na miongoni mwao wanafunzi 1097 (1.9%) walipata alama zote 20. Chati ya 5 inaonesha kufaulu kwa wanafunzi kwa asilimia.




**Chati ya 5**: *Alama za Wanafunzi kwa Asilimia Katika Swali la 5*

Uchambuzi uliofanywa katika majibu ya wanafunzi kwenye swali hili unaonesha kuwa kiwango cha kufaulu ni cha wastani kwa kuwa wanafunzi 28,971 (51.1%) kati ya 56,708 waliojibu swali walipata alama 5 hadi 20 ambazo zilikuwa ni alama za kufaulu katika swali hili. Wanafunzi hawa waliweza kupanga kwa usahihi sentensi tano za kipengele (a) zilizohusu

Historia ya kushuka kwa Qur'an kwa Mtume (s.a.w) na pia kipengele (b) kilichohusu ubashiri wa ushindi na kuangamia kwa maadui wa Uislamu kama unavyothibitishwa ndani ya Qur'an. Hata hivyo alama za wanafunzi hawa zilitofautiana kutokana na uwezo tofauti wa wanafunzi wa kupanga sentensi kwa usahihi. Wanafunzi 1097 (1.9) walipata alama zote 20 kwa sababu walikuwa na uelewa wa mada za Qur'an hasa katika Historia ya kushushwa na kuhifadhiwa Qur'an na pia kusoma na kutafsiri Sura zilzoteuliwa. Wanafunzi hawa pia waliweza kufuata maelekezo ya swali kwa kupanga sentensi ya kwanza hadi ya tano kwa kila kipengele kama inavyotakiwa. Kielelezo 5.1 kinaonesha mfano wa jibu la mwanafunzi aliyeweza kupanga kwa usahihi nukuu kwa vipengele vyote viwili.

**Kielelezo 5.1**

5. Nukuu zifuatazo hazikupangwa katika mtiririko unaotakiwa. Panga nukuu hizo katika mpangilio sahihi ili kupata maana iliyokamilika.

(a) Kwa mujibu wa Hadithi, historia ya kushuka kwa Qur'an kwa Mtume (s.a.w) kulizingatia mtiririko ufuatao:

4 (i) Kisha kutoka humo ikashushwa kidogo kidogo kwa Mtume (s.a.w) kupitia kwa malaika Jibril (a.s) kwa kipindi chote cha utume cha miaka 23.

5 (ii) Aya za mwanzo kumshukia Mtume (s.aw) ni aya tano za mwanzo za suratul-'Alaq.

1 (iii) Kabla ya Mtume (s.a.w) hajaanza kushushiwa Qur'an kupitia kwa malaika Jibril (a.s) alikuwa akipata wahyi kwa njia ya ndoto.

3 (iv) Kutoka Lawhi Mahfudh Qur'an ilishushwa mpaka uwingu wa kwanza.

2 (v) Qur'an yote kwa ujumla imehifadhiwa katika ubao mtukufu wa Allah (s.w) ulio katika Arshi yake.

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
|---|---|---|---|---|
| iii | v | iv | i | ii |

(b) Ubashiri wa ushindi na kuangamia kwa maadui wa Uislamu unathibitishwa ndani ya Qur'an katika aya zifuatazo:

5 (i) (Kama kwamba) shingoni mwake iko kamba iliyosokotwa (anayochukulia kuni za fitna).

1 (ii) Pana kuangamia mikono miwili ya Abu Lahab! Naye amekwisha angamia.

4 (iii) Na mkewe, mchukuzi wa kuni (za fitina), fatani anayefitinisha watu wasiingie katika dini (ataingia naye moto huo).

3 (iv) Hayatamfaa mali yake wala alivyovichuma.

3 (v) (Atakapokufa) ataingia moto wenye mwako (mkubwa kabisa).

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
|---|---|---|---|---|
| ii | iv | v | iii | i |

Kielelezo 5.1 kinaonesha mfano wa jibu la mwanafunzi aliyeweza kupanga kwa usahihi nukuu zilizopo kwenye vipengele vyote viwili (a) na (b) hivyo kuleta mtiririko wenye kuleta maana katika kila kipengele.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa, wanafunzi 24,066 waliojibu swali hili walipata alama za wastani kwa sababu waliweza kupanga kwa usahihi kipengele (b) lakini walishindwa kupanga kwa usahihi kipengele (a). Sababu kubwa iliyowafanya wanafunzi wengi kushindwa kupanga kwa usahihi kipengele (a) ni kutokana na ukweli kuwa nukuu zake hazikutokana na tafsiri moja kwa kwa moja ya Sura ya Qur'an bali ni maelezo ya hatua za kuteremshwa kwa Qur'an. Hii iliwafanya wanafunzi wengi wasio na maarifa ya kutosha ya Historia ya kushuka kwa Qur'an kwa Mtume (s.a.w) kushindwa kupanga kwa usahihi hatua hizo bali walichanganya mtiririko wa hatua hizo. Hii ilisababisha wanafunzi hawa kukosa alama katika kipengele (a) kwa kushindwa kupanga kwa usahihi. Kwa mfano, wanafunzi wengi walipanga sentensi ya (v) kuwa ndio ya kwanza wakati sentensi hiyo ni pili. Hii ina maana kuwa wanafunzi hawa walipata alama kwa kuweza kupanga kipengele (b) peke yake kilichohusu aya za Sura ya Qur'an ya Lahab.

Wanafunzi 6,299 (11.1%) hawakuwa na maarifa ya mada ya Qur'an hasa katika kushushwa na kuhifadhiwa kwa Qur'an na kusoma na kutafsiri Sura zilizoteuliwa. Wanafunzi hawa walishindwa kujibu vipengele vyote viwili. Ili kujibu swali hili mwanafunzi alihitaji kuwa na maarifa ya kutosha ya mada ya Qur'an, maarifa ambayo wanafunzi hawa hawakuwa nayo. Vilevile baadhi ya wanafunzi hawa walishindwa kufuata maelekezo ya swali na kuamua kujaza majibu kwa namna isiyo sahihi kwa kutumia namba za kiarabu au herufi. Wanafunzi wengine waliandika sentensi kwenye sehemu ya kujibia. Wengine pia waliacha wazi bila kujaza chochote kwenye vipengele vyote viwili. Kielelezo 5.2 kinaonesha mfano wa jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kwa usahihi.

**Kielelezo 5.2**

5. Nukuu zifuatazo hazikupangwa katika mtiririko unaotakiwa. Panga nukuu hizo katika mpangilio sahihi ili kupata maana iliyokamilika.

(a) Kwa mujibu wa Hadithi, historia ya kushuka kwa Qur'an kwa Mtume (s.a.w) kulizingatia mtiririko ufuatao:

(i) Kisha kutoka humo ikashushwa kidogo kidogo kwa Mtume (s.a.w) kupitia kwa malaika Jibril (a.s) kwa kipindi chote cha utume cha miaka 23.

(ii) Aya za mwanzo kumshukia Mtume (s.aw) ni aya tano za mwanzo za suratul-'Alaq.

(iii) Kabla ya Mtume (s.a.w) hajaanza kushushiwa Qur'an kupitia kwa malaika Jibril (a.s) alikuwa akipata wahyi kwa njia ya ndoto.

(iv) Kutoka Lawhi Mahfudh Qur'an ilishushwa mpaka uwingu wa kwanza.

(v) Qur'an yote kwa ujumla imehifadhiwa katika ubao mtukufu wa Allah (s.w) ulio katika Arshi yake.

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
|---|---|---|---|---|
| ii | v | iv | iii | i |

(b) Ubashiri wa ushindi na kuangamia kwa maadui wa Uislamu unathibitishwa ndani ya Qur'an katika aya zifuatazo:

(i) (Kama kwamba) shingoni mwake iko kamba iliyosokotwa (anayochukulia kuni za fitna).

(ii) Pana kuangamia mikono miwili ya Abu Lahab! Naye amekwisha angamia.

(iii) Na mkewe, mchukuzi wa kuni (za fitina), fatani anayefitinisha watu wasiingie katika dini (ataingia naye moto huo).

(iv) Hayatamfaa mali yake wala alivyovichuma.

(v) (Atakapokufa) ataingia moto wenye mwako (mkubwa kabisa).

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
|---|---|---|---|---|
| iv | iii | i | ii | v |

Kielelezo 5.2 kinaonesha mfano wa jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kupanga kwa usahihi nukuu zilizopo kwenye vipengele (a) na (b) kwa usahihi.


## 2.3 SEHEMU C: FIQH

Sehemu hii ilihusu mada za Fiqh na ilikuwa na maswali mawili yenye jumla ya alama 40. Swali la sita lilikuwa ni la majibu mafupi ambapo mwanafunzi aliulizwa vipengele vitano vifupi (a, b, c, d na e). Mwanafunzi alitakiwa aidha ataje, aeleze maana au aorodheshe majibu. Swali la 7 lilikuwa la insha ambapo mwanafunzi alitakiwa aandike insha kuhusu Hijja.

### 2.3.1 Swali la 6: Fiqh - Kujibu kwa Ufupi

Swali lilihusu mada za *Fiqh* ambapo kipengele (a) kilipima uelewa wa mwanafunzi kuhusu lengo la kuumbwa mwanadamu na alitakiwa kutaja mambo manne ambayo mwanadamu akiyafanya atakuwa ametekeleza sehemu ya lengo la kuumbwa kwake hapa duniani. Kipengele (b) kilihusu kusimamisha Swala na mwanafunzi alitakiwa kutoa maana ya istilahi ya kadha kisheria, hukumu yake katika Swala na kuorodhesha mambo mawili ambayo msafiri ameruhusiwa katika kutekeleza Swala tano za Faradh. Kipengele (c) kilihusu mambo ya lazima ya kumfanyia maiti wa kiislamu ambapo mwanafunzi alitakiwa kutaja mambo manne ambayo yanapaswa kuzingatiwa na muoshaji wa maiti ya Kiislamu. Kipengele (d) kilihusu Nguzo ya Funga na mwanafunzi alitakiwa kueleza maana ya funga kilugha na kisheria. Kipengele (e) kilihusu Hijja ambapo mwanafunzi alitakiwa kueleza maana na aina tatu za Tawafu. Swali lilikuwa na vipengele vitano (a) – (e). na lilimtaka mwanafunzi kutoa majibu mafupi. Kila kipengele kilikuwa na alama 4 ambapo swali zima lilikuwa na jumla ya alama 20.

Wanafunzi 56,585 kati ya 56,749 waliofanya upimaji walijibu swali hili. Wanafunzi 465 (0.8%) walipata alama 0, wanafunzi 12,969 (22.9%) walipata alama 0.5 hadi 5.5, wanafunzi 33,906 (60%) walipata alama 6 hadi 12.5. Wanafunzi 9,245 (16.3%) walipata alama 13 hadi 20, miongoni mwao wanafunzi 13 tu walipata alama zote 20. Chati ya 6 inaonesha kufaulu kwa wanafunzi kwa asilimia.




**Chati ya 6**: *Alama za Wanafunzi kwa Asilimia Katika Swali la 6*

Kwa ujumla kiwango cha kufaulu kwa wanafunzi katika swali hili ni kizuri kwani wanafunzi 43,151 (76.3%) walipata alama 6 hadi 20 ambazo zilikuwa ni alama za kufaulu kwenye swali hili. Wanafunzi 9,245 (16.3%) walipata alama za juu (13 hadi 20) kwa sababu walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Fiqh na waliweza kujibu kwa usahihi vipengele vyote vitano vya swali hili. Hata hivyo baadhi ya maelezo yao hayakuwa ya kutosha na wengine walijibu mambo machache kuliko ilivyotakiwa kwa kila kipengele na walishindwa kupata alama zote 20 za swali hili. Wanafunzi 13 tu ndiyo waliweza kupata alama zote 20 kwenye swali hili kwa kuwa waliweza kujaza vipengele vyote vitano kwa usahihi na kwa mujibu wa ilivyotakiwa kwa kila kipengele. Vipengele vilivyojibiwa vizuri na wanafunzi hawa ni (c) na (d).

Katika kipengele (c) wanafunzi hawa waliweza kutaja mambo manne ambayo yanapaswa kuzingatiwa na muoshaji wa maiti ya Muislamu. Mambo ambayo wanafunzi waliyataja ni pamoja na maiti ya kiume ioshwe na mwanamume na maiti ya kike ioshwe na mwanamke. Vilevile ni sunnah mume kumuosha mke na mke kumuosha mume, ni mtu mmoja tu anayeosha na mwingine/wengine wakumpa msaada pale itakapohitajika, kufahamu masharti ya kuosha maiti kama vile sifa za muoshaji na mahala pa kuoshea namna ya kumuosha. Kufahamu nguzo na Sunnah za kuosha kama vile nia, kuenea kwa maji mwili mzima na Sunnah ya kumuosha mara tatu au zaidi.

Katika kipengele (d) wanafunzi hawa waliweza kueleza maana ya funga kilugha na kisheria na wengi walieleza kuwa funga kilugha ni kujizuia kufanya jambo lolote la kawaida na funga kisheria ni kujizuia kula, kunywa, kujamii na kuingiza kitu chochote katika matundu ya mwili na kujizuilia kumuasi Allah (s.w) kuanzia alfajiri ya kweli mpaka kuingia magharibi. Kielelezo 6.1 kinaonesha mfano wa jibu la mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi vipengele vyote vitano.

**Kielelezo 6.1**

6. Jibu maswali yote kwa ufupi.

(a) Taja mambo manne ambayo mwanadamu akiyafanya atakuwa ametekeleza sehemu ya lengo la kuumbwa kwake hapa duniani.

(i) Kusimamisha swala tano

(ii) Kufunga mwezi mtukufu wa Ramadhan

(iii) Kutoa Zakkat

(iv) Kuhiji

(b) (i) Nini maana ya "kadha" kisheria na ipi hukumu yake katika Swala?

Kadha kisheria ni kulipa au kufidia katika ibada uliyosahau kufanya mfano Swala. Hukumu yake katika swala ni kulipa swala hiyo mara tu baada ya kutoka kwenye udhuru huo mfano kulala, safari

(ii) Orodhesha mambo mawili ambayo msafiri ameruhusiwa katika kutekeleza Swala tano za faradh.

- Kuunganisha swala. Mfano akaswali Adhuhuri na Alasiri kwa pamoja
- Kufupisha swala mfano Adhuhuri akaswali rakaa mbili badala ya nne

(c) Taja mambo manne muhimu ambayo yanapasa kuzingatiwa na muoshaji wa maiti ya Muislamu.

(i) Anatakiwa azingatie usiri (asiwe mwenye kusema mabaya ya maiti

(ii) Muoshaji anatakiwa awe na Muislamu

(iii) Muoshaji anatakiwa awe vitu ambavyo vitamzuia kumshika maiti moja kwa moja

(iv) Anatakiwa awe na elimu ya kutosha juu ya shughuli ya uoshaji wa maiti

(d) (i) Nini maana ya funga kilugha?

Funga kilugha ni kujizuilia (kujizuia). Mfano mtu anaweza akajizuia kuongea, kutoa maneno mabaya, kula chakula fulani na kufanya kitu fulani akipendacho. Hii yote ni maana ya funga kilugha

(ii) Nini maana ya funga kisheria?

Funga kisheria ni kujizuilia kula, kunywa na mambo yote yanayobatilisha swaum kuanzia jua linapochomoza hadi litakapozama mfano funga ya Ramadhan (faradh) na funga za sunnah mfano funga ya Arafa, funga ya siku sita za shawwal na funga za jumatatu na Alhamisi

(e) (i) Nini maana ya Tawaf?

Tawaf ni kitendo cha kuzunguka kaaba mara saba kuanzia kwenye jiwe jeusi

(ii) Taja aina tatu za Tawaf.

- Tawaful - Ifadhwa
- Tawaful - Qudum
- Tawaful - Widaa.

Kielelezo 6.1 kinaonesha mfano wa jibu la mwanafunzi aliyeweza kutaja mambo ambayo mwanadamu akiyafanya atakuwa ametekeleza sehemu ya lengo la kuumbwa kwake hapa duniani, maana ya kadha kisheria na hukumu yake, mambo muhimu ya kuzingatiwa na muoshaji maiti, maana ya funga kilugha na kisheria na maana na aina za Tawafu.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa, wanafunzi 33,906 (59.9%) kati ya 56,585 waliojibu swali hili na kupata alama za wastani. Baadhi ya wanafunzi hao walijibu baadhi ya vipengele na kuacha

vingine kwa mfano mwanafunzi mmoja aliweza kujibu kipengele (a) kinachohusu mambo manne ya kutekeleza lengo la kuumbwa na kipengele (b) kinachohusu kinachusu maana ya kadha sharia na hukumu yake katika Swala. Hata hivyo mwanafunzi huyo aliacha kujibu vipengele (c), (d) na (e) hivyo kupata alama za wastani. Vilevile baadhi ya wanafunzi walipata alama za wastani kwa sababu walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi kwa baaddhi ya vipengele, hivyo kushindwa kupata alama za juu. Kwa mfano mwanafunzi mmoja alijibu kipengele (a) na (b) (i) na (e) kwa usahihi lakini alishindwa kujibu (b) (ii), (c) na (d). Baadhi walishindwa kujibu vipengele (a), (b), (e) kwa usahihi.

Wanafunzi 13,434 (23.7%) walipata alama za chini (0 hadi 5.5) kwa kuwa hawakuwa na maarifa ya kutosha ya mada ya Sunnah na Hadithi. Vipengele ambavyo havikujibiwa kwa usahihi na wanafunzi wengi ni kipengele (a), (b) na (e).

Katika kipengele (a) watahiniwa walitakiwa kutaja mambo ambayo mwanadamu akiyafanya atakuwa ametekeleza sehemu ya lengo la kuumbwa kwake hapa duniani. Baadhi ya wanafunzi hawa walitaja nguzo nne za kiiislamu kati tano ambazo ni shahada, Swala, zaka, funga na Hijja. Pia wanafunzi wachache walitaja nguzo za Imani kama vile, kumuabudu Allah (s.w), malaika wake, kuamini mitume wake na kuamini siku ya mwisho. Hii ilisababisha wanafunzi hawa kushindwa kupata alama katika kipengele hiki. Majibu sahihi ya kipengele hiki ni kutekeleza nguzo za Uislamu, kutekeleza nguzo za Imani, kuamrisha mema na kukataza maovu, kutekeleza nguzo za Ihsani, kupigana jihadi, kutafuta Elimu, kuchuma na kutumia mali kwa njia ya halali na kusimamisha uadilifu.

Kipengele (b) kilimtaka mwanafunzi kueleza maana ya kadha kisheria na hukumu yake katika Swala na pia kuorodhesha mambo mawili ambayo msafiri ameruhusiwa katika kutekeleza Swala tano za faradh. Kutokana na kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Swala, wanafunzi hawa walishindwa kueleza maana ya kadha kisheria na hukumu yake na hivyo kutoa majibu ya kubuni ambayo hayahusiani na neno kadha. Mfano wa majibu hayo ya kubuni yaliyotolewa na wanafunzi hawa ni kama vile; kadha ni kuwa katika swala ukiwa unafikiria vitu vya nje, ni kitendo cha kunyanyua mikono katika kubadili vitendo vya swala, ni kipengele cha maudhi ya swala, ni taaluma ya kisheria ya kiislamu na ni matendo ya ziada ya Sunnah. Wanafunzi wengi pia waliacha sehemu ya kujibia wazi bila ya

kuandika chochote. Vilevile ni wanafunzi wachache sana walioweza kuorodhesha mambo ambayo msafiri ameruhusiwa katika kutekeleza Swala tano za faradh.

Katika kipengele (e) kilichomtaka mwanafunzi kueleza maana na aina za Tawaf, wanafunzi hawa walishindwa kabisa kutaja aina za tawafu ingawa waliweza kueleza maana ya tawafu. Baadhi ya wanafunzi walichanganya Tawafu na faradh na matokeo yake badala ya kutaja aina za tawafu, wanafunzi hawa walitaja aina za faradhi hivyo kutaja tawafu aini na tawafu kifaya. Baadhi ya wanafunzi walitaja tawafu za matamshi, vitendo na moyoni. Aina za tawafu zipo tatu ambazo ni tawaful ifadha, tawaful Qudum na tawaful widaa.

Wanafunzi waliopata alama 0 walishindwa kujibu vipengele vyote vitano kwa usahihi kutokana na kutokuwa na maarifa ya kutosha kwenye mada za Fiqh. Baadhi yao waliacha wazi sehemu za kujibia bila kuandika chochote na hivyo kupata alama 0. Kielelezo 6.2 kinaonesha mfano wa jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kwa usahihi vipengele vyote vitano vya swali hili.

**Kielelezo 6.2**

5. Jibu maswali yote kwa ufupi.

(a) Taja mambo manne ambayo mwanadamu akiyafanya atakuwa ametekeleza sehemu ya lengo la kuumbwa kwake hapa duniani.

(i) Kudhini

(ii) Kuto kumuabudu mtume (S.a.w)

(iii) Kufanya mambo kwa kumkeuka mwenyezimungu.

(iv) Kuingia kanisani na wakati wewe ni muislamu.

(b) (i) Nini maana ya "kadha" kisheria na ipi hukumu yake katika Swala?

Kadha ni Kuto kumuabudu Allah na kuto fanya jitihada yoyote ile ya kusoma Qur an.

Hukumu ni Kumuabudu Allah popote pale alipo mwanadamu yoyote yule.

(ii) Orodhesha mambo mawili ambayo msafiri ameruhusiwa katika kutekeleza Swala tano za faradh.

- Msafiri akiwa amesafiri umbali mrefu anaweza kuruhusiwa kuto kuswali swala ya farodh.
- Msafiri akiwa na mizigo mingi mkono ni na hivyo hato weza kuruhusiwa.

(c) Taja mambo manne muhimu ambayo yanapasa kuzingatiwa na muoshaji wa maiti ya Muislamu.

(i) Anatakiwa asiteme mate huku akiwa anaosha maiti.

(ii) Unatakiwa usicheke huku ukiwa unaosha maiti.

(iii) Unatakiwa usiongee na mtu huku ukiwa unaosha maiti.

(iv) Unatakiwa uwe na udhu kabla haujaanza kumuosha maiti.

(d) (i) Nini maana ya funga kilugha?

funga ni ufungaji wa mwezi mtukufu wa ramadhani.

(ii) Nini maana ya funga kisheria?

funga ni kufunga kwa mwezi wa ramadhani kwa siku mpaka sikukuu ikifika na huwa wanafunga kuanzia asubuhi mpaka jioni saa kumi na mbili na nusu ndio wanafungulia na kuanza kufuturu kitu chochote kile ulichojaaliwa nacho.

(e) (i) Nini maana ya Tawaf?

~~Tawafe ni mtume wa Qur'an.~~

Tawaf ni kukaa chini.

(ii) Taja aina tatu za Tawaf.


- Tawafu maana
- Tawafu mkunjufu
- Tawafu mfoofu.

Kielelezo 6.2 kinaonesha mfano wa jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kujibu vizuri mambo ambayo mwanadamu akiyafanya atakuwa ametekeleza sehemu ya lengo la kuumbwa kwake hapa duniani, maana ya kadha kisheria na hukumu yake, mambo muhimu ya kuzingatiwa na muoshaji maiti, maana ya funga kilugha na kisheria na maana na aina za Tawafu.

### 2.3.2 Swali la 7: Fiqh - Insha

Swali hili lilihusu kipengele cha Hijja katika mada ya Fiqh. Mwanafunzi alitakiwa aeleze sifa nne za Muislamu ambaye anaweza kutekeleza Ibada ya Hijja kama inavyotakiwa. Swali lilikuwa la insha na lenye alama 20.

Wanafunzi 51,315 (90.4%) kati ya 56,749 waliofanya upimaji walijibu swali hili. Takwimu zinaonesha kuwa wanafunzi 15,634 (30.5%) walipata alama 0, wanafunzi 20,840 (40.6%) walipata alama 0.5 hadi 5.5 na wanafunzi 11,195 (21.8%) walipata alama 6 hadi 12.5. Wanafunzi waliopata alama 13 hadi 20 walikuwa 3,646 (7.1%) na miongoni mwao wanafunzi 135 (0.2%) walipata alama zote 20. Chati ya 7 inaonesha kufaulu kwa wanafunzi kwa asilimia.




**Chati ya 7**: *Alama za Wanafunzi kwa Asilimia Katika Swali la 7*

Uchambuzi uliofanywa kwenye majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa kiwango cha kufaulu kwa wanafunzi kwenye swali hili kilikuwa dhaifu. Wanafunzi 14,841 (28.9%) kati ya 51,315 waliojibu swali hili walipata kuanzia alama 6 hadi 20. Wanafunzi 1,195 (21.8%) walipata alama za wastani kwa sababu walichanganya sifa sahihi na ambazo sio sahihi za Muislamu ambaye anaweza kutekeleza ibada ya Hijja kama inavyotakiwa mfano wa sifa zisizo sahihi ambazo zilichanganywa na sifa sahihi ni kama vile; awe mcha Mungu, awe mkarimu kwa watu, awe na tabia nzuri asiwe mwenye kugombana lazima azunguke Kaaba na lazima apande vilima viwili na kama ni mwanamke asiwe katika hedhi au Nifasi na awe ameruhusiwa na mumewe. Baadhi yao pia walishindwa kuandika insha


kama swali linavyoelekeza, waliorodhesha majibu katika mtindo wa nambari. Wanafunzi 20,840 (71.1%) walipata alama za chini (0 hadi 5.5) kwa sababu walishindwa kueleza sifa nne za Muislamu ambaye anaweza kutekeleza ibada ya Hijja kama inavyotakiwa. Wanafunzi 15,634 (30.5%) walipata alama 0 kwa sababu walishindwa kuelewa matakwa ya swali na hivyo kuandika nguzo za Uislamu badala ya sifa za Muislamu ambaye anaweza kutekeleza ibada ya Hijja kama inavyotakiwa. Vilevile, baadhi yao waliandika sifa za mcha Mungu kama vile, anapotajwa Allah (s.w) nyoyo hujaa hofu, humtegemea Allah (s.w) katika kila jambo, husimamisha swala na kutoa zakat na humuamudu Allah (s.w) kikamilifu. Wanafunzi wengine waliandika vitendo vya Hijja kama vile Ihram, Tawafu, achunge mipaka ya Mwenyezi Mungu na kwenda Hijja katika wakati wake maalum. Majibu haya ambayo sio sahihi yanaonesha kuwa wanafunzi hawa hawakuwa na maarifa ya kutosha kwenye mada ya Hijja na hivyo walishindwa kupata alama za juu. Kielelezo 7.1 kinaonesha mfano wa jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kueleza sifa nne za Muislamu ambaye anaweza kutekeleza ibada ya Hijja kama inavyotakiwa.

**Kielelezo 7.1**

7. Elezea sifa nne za Muislamu ambaye anaweza kutekeleza ibada ya Hija kama inavyotakiwa.

Hija Ni moja wapo ya nguzo za kislamu na ni nguzo ya tano: hija Ni kitendo cha kwenda kuhiji: Na hujiwa kipindi cha Dhul hijja na ni faradhi kwenda kuhiji kwa kila mwenye uwezo. na ukienda kuhiji ni lazima uvae Ihram ni vazi ambalo huva liwa wakati wa hijja au hijjat pale anapokwenda kuhiji au kipindi cha umra: umra ni kitendo cha kufanya Ibada ndogo wasote na ni sunnah na hufa nyika na mtu yeyote yule mwenye uwezo. zifuatazo ni sifa nne ambazo anaweza kutekeleza Ibada ya Hija kama Inavyotakiwa.

Kuvaa Ihram: Ihram ni vazi ambalo huvaliwa na hija au hijjat pale anapokwenda kuhiji au kufanya umra. na kuna aina za Ihram kuna Ihram ya Mwanaume ambayo Ihram ya mwanaume ni shuka jeupe ambalo hufunika bega la kulia na kuacha bega la kushoto. na Ihram ya mwanamke ni nguo yoyote ile lakini isiwe na mapambo na isionyeshe umbo.


Kutofanya tendo la ndoa: Kutofanya tendo la ndoa ya ukifanya tendo la ndoa wakati upo katika hija hija yako hairusiwi na wala haipokelewi na utalazimika kufunga miezi miwili mfululizo au kuwalisha masikini sitini au kumlisha masikini kwa siku sitini.

Kupunguza nywele: hairusiwi kupunguza nywele au kung'oa nywele na ukifanya hivyo hija yako haitakubaliwa na wala haitapokelewa.

Kufanya ibada zote za hijja: Nilazima ufanye ibada zote za hijja na ukiacha ata moja unaanza tena upiya na kama hauna uwezo wa kufanya ibada zote basi mtu yeyote yule mwenye nguvu atabidi akubebe au akuweke katika vibaisikeli ili ukamilishe ibada ya hijja. hijja nimuhimu sana kwa sababu pindi ukienda kufanya hijja unakuwa unasamehewa madhambi zako zote unakuwa kama mtoto mdogo yule aliye zaliwa leo. na katika hijja kunamambo hayaruhusiwi kufanya: kama kufanya tendo la ndoa wakati upo katika hija, kukata nywele, kukata kucha na kutovaa Ihram, kusengenya, kusema uongo, kuingia katika makundi machafu. Tunatakiwa kama tukienda kuhijji kwa kila mwenye uwezo anabidi apuka ne na mambo hayo.

Kielelezo 7.1 kinaonesha mfano wa majibu ya mwanafunzi aliyeeleza matendo ya Hijja na mipaka ya Ihram badala ya kueleza sifa za Muislamu ambaye anaweza kutekeleza ibada ya Hijja kama inavyotakiwa.

Uchambuzi zaidi uliofanywa katika majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa wanafunzi 3,646 (7.1%) walipata alama za juu (13 hadi 20) kwa sababu walikuwa na maarifa ya kutosha kujibu kwa usahihi kuhusu mada ya Fiqh. Wanafunzi hawa waliweza kueleza sifa nne za Muislamu ambaye anaweza kutekeleza ibada ya Hijja kama inavyotakiwa. Sifa zilizotajwa na wanafunzi hawa ni pamoja na awe baleghe, awe na akili timamu, awe muungwana na sio mtumwa, mwenye uwezo wa kifedha na kiafya, asiowekewa kizuizi njiani na kama Muislamu huyo ni mwanamke aongozane na maharim. Hata hivyo alama za wanafunzi zilitofautiana kutegemea na idadi ya sifa zilizotakiwa na maelezo yake. Wanafunzi

waliopata alama zote 20 waliweza kufuata matakwa ya swali pamoja na kuwa na mpangilio mzuri wa insha kwa kuandika sehemu ya utangulizi, kiini na hitimisho na pia kuwa na maarifa ya mada ya Hijja yaliyowawezesha kuandika maelezo ya kutosha na kutoa mifano kwa kila sifa. Kielelezo cha 7.2 kinaonesha mfano wa jibu la mwanafunzi aliyeweza kujibu swali hili kwa usahihi kwa kuandika sifa nne za Muislamu ambaye anaweza kutekeleza ibada ya Hijja kama inavyotakiwa na pia kwa kuwa na mpangilio mzuri wa insha.

**Kielelezo 7.2**

7. Elezea sifa nne za Muislamu ambaye anaweza kutekeleza ibada ya Hija kama inavyotakiwa.

Wenye akili timamu: Muislamu anayetaka kwenda Makkah kuhiji anatakiwa awe amekamilika kiakili asiwe chizi. Anaweza kwenda akaharibu masharti ya hija na nguzo zake kwa sababu atakuwa ajatimia akili vizuri kwahiyo mtu ambaye ajatimia akili timamu anatakiwa asiende kuhiji.

Wasiwe na vizuizi njiani. Muislamu anayetaka kwenda kuhiji anatakiwa asiwe na kizuizi chochote njiani. Kizuizi kina maana ya kitu chochote kisichoweza kuharibu au kugomesha ~~shafa~~ safari ya kwenda kuhiji kwa mfano tuseme nauli ya kwenda haitoshi hiyo ni mojawapo ya kizuizi atakachokipata ndio maana nilitangulia kusema uwe na uwezo. pia ni vizuri zaidi kwenda na Magharimu wao.

Hivyo basi ni vizuri ukiwa umetosheleza sifa zote za mtu anayetaka kwenda hija ili kuepusha usumbufu nje ya usumbufu kisheria haitakiwi unatakiwa uwe umetosheleza ~~shif~~ sifa zote za mwenye kuhiji.

Kielelezo 7.2 kinaonesha mfano wa jibu la mwanafunzi aliyeeleza kwa usahihi sifa nne za Muislamu ambaye anaweza kutekeleza ibada ya Hijja kama inavyotakiwa.

## 3.0 UCHAMBUZI WA KUFAULU KWA KILA MADA

Kiwango cha jumla cha kufaulu kwa mada katika upimaji wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu ni cha wastani. Mada zilizopimwa katika upimaji huu ni *Sunnah na Hadithi*, *Tawhiid*, *Tarekh, Qur'an* na *Fiqh*. Uchambuzi wa takwimu za matokeo ya wanafunzi katika mada mbalimbali katika upimaji wa somo hili unaonesha kiwango kizuri cha kufaulu katika mada za *Tawhiid* iliyokuwa na maswali ya kuoanisha maneno na sentensi na kujibu kweli au si kweli; mada ya *Sunnah na Hadithi* iliyokuwa na swali la kuchagua jibu sahihi na mada ya *Tarekh*. Mada hizo zilikuwa na viwango vya kufaulu vya asilimia 91.9, 83.2 na 69.1 mutawalia. Aidha wanafunzi walifaulu kwa wastani katika mada ya *Fiqh (52.6%)* iliyokuwa na maswali ya majibu mafupi na Insha na Mada ya *Qur'an (51.1%)* iliyokuwa na swali la kupanga nukuu katika mpangilio sahihi ili kupata maana iliyokamilika.

Uchambuzi katika majibu ya wanafunzi umebaini kuwa sababu kubwa za wanafunzi kufaulu kwa kiwango kizuri katika mada za *Tawhiid*, *Sunnah na Hadithi* na *Tarekh* ni kutokana na kuwa na maarifa ya kutosha katika mada hizo na kuelewa matakwa ya swali. Vilevile kufaulu kwa kiwango cha wastani katika mada za *Qur'an* na *Fiqh* inatokana na kutokuwa na maarifa ya kutosha katika mada hizi. Hii ilisababisha wanafunzi kuandika maelezo yasiyojitosheleza, kuchanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi na kuacha wazi baadhi ya vipengele vya mada ya *Fiqh* katika maswali ya majibu mafupi. Aidha baadhi ya wanafunzi walipata alama za chini kwa kutofuata maelekezo ya swali, kwa kuandika katika mfumo wa namba au kwa kuorodhesha majibu badala ya kuandika katika mfumo wa insha katika swali lililohitaji kuandikwa kwa insha. Muhtasari wa takwimu kwa wastani wa kila mada umeoneshwa kwenye kiambatisho ambapo rangi ya njano inaonesha kufaulu kwa wastani na rangi ya kijani inaonesha kiwango kizuri cha kufaulu kwa swali husika.

## 4.0 HITIMISHO

Kwa ujumla kiwango cha kufaulu kwa wanafunzi katika FTNA 2018 kwenye somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu ni cha wastani wa asilimia 49.71. Uchambuzi huu ulionesha changamoto mbalimbali ambazo hazina budi kutatuliwa kama vile; wanafunzi kutofuata maelekezo ya swali, kushindwa kutoa maelezo yanayojitosheleza, kuandika majibu kwa mtindo wa namba au herufi kwenye maswali yanayohitaji muundo wa insha hivyo kushindwa kupanga majibu katika sehemu tatu za utangulizi, kiini na

hitimisho na pia uelewa mdogo wa mada mbalimbali na hasa mada ya *Qur'an*. Ili kuinua zaidi kiwango cha kufaulu kwa mada zote katika upimaji ujao, jitihada zinahitajika katika ufundishaji na ujifunzaji ili kuwajengea wanafunzi ujuzi wa kuandika insha na kujenga hoja. Ni muhimu pia kujua Historia ya kushushwa kwa Qur'an, kusoma na kuhifadhi aya za Qur'an ikizingatiwa kuwa Qur'an ndio msingi wa dini ya Kiislamu.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuinua kiwango cha kufaulu katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu yafuatayo yanapendekezwa:

(a) Walimu wawaongoze wanafunzi katika vikundi kusoma, kuhifadhi na kutafsiri Qur'an hasa Sura zilizoteuliwa. Wanafunzi wapewe kazi ya kukusanya taarifa kutoka katika vitabu mbalimbali vinavyohusu Historia ya kushushwa Qur'an kwa jumla ikiwa pamoja na namna ilivyoshushwa, kukusanywa na kuhifadhiwa katika kitabu cha Qur'an hadi sasa.

(b) Ili kuwajengea uwezo wa kujibu maswali ya kujieleza na insha kila mwalimu anapomaliza kufundisha mada za *Fiqh* awape wanafunzi mazoezi yanayohusu kutoa maelezo na namna ya kuandika insha. Pia wanafunzi wapewe kazi za kujadili kivikundi na baada ya majadiliano wawasilishe darasani ili kupata mrejesho sahihi.

(c) Ili kuwajengea wanafunzi uwezo wa kutambua matakwa ya swali na uwezo wa kuibua majibu sahihi, mwalimu anapomaliza kufundisha mada awape wanafunzi mazoezi mengi kisha afanye masahihisho darasani.

**Kiambatisho**

## UCHAMBUZI WA KUFAULU KWA WANAFUNZI KATIKA MADA

| Na. | Mada | Kufaulu kwa Kila Swali | | Asilimia ya Wanafunzi waliopata Wastani wa Alama 30 au Zaidi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Nambari ya Swali | Asilimia ya Kufaulu | | |
| 1 | Tawhiid | 3 | 98.1 | 91.95 | Vizuri |
| | | 2 | 85.8 | | |
| 2 | Sunnah na Hadithi | 1 | 83.2 | 83.2 | Vizuri |
| 3 | Tarekh | 4 | 69.1 | 69.1 | Vizuri |
| 4 | Fiqh | 6 | 76.3 | 52.6 | Wastani |
| | | 7 | 28.9 | | |
| 5 | Qur'an | 5 | 51.1 | 51.1 | Wastani |
| **Wastani wa Jumla wa Kufaulu** | | | | **49.71** | **Wastani** |